

Tarehe 05.04.2024

**TANGAZO LA ZABUNI YA UTOAJI HUDUMA YA MAFUTA YA DIESEL NA PETROL KWA
MAGARI MAKUBWA NA MADOGO YA KCU (1990) LTD MSIMU 2024/2025**

Zabuni na: KCU/Z/2024/2025/03

1. KCU (1990) LTD Inamiliki magari madogo na makubwa ambayo huyatumia katika kazi za kiofisi na shughuli za kuhudumia zao la kahawa katika msimu. Kwa vile magari haya yanatumia nishati ya mafuta ya Diesel na petrol, kituo cha mafuta kitahitajika kutoa huduma hii kwa msimu 2024/2025.
2. Maombi yanakaribishwa kutoka kwa wamiliki/waendeshaji wa vituo vya mafuta hapa Bukoba mjini/Manispaa kwa ajili kutoa huduma ya mafuta ya diesel na petroli kwa magari ya KCU (1990) Ltd.
3. Mwombaji sharti awe na kituo cha mafuta, chenye leseni na usajili wa TIN/VAT yakufanya biashara ya mafuta Bukoba na kutaja mahali kilipo.
4. Mwombaji awe tayari kutoa huduma kulingana na bei elekezi za EWURA.
5. Maombi yataje suala la uwepo wa usalama wa magari yanapokuwa yanajaza mafuta kwenye kituo cha mafuta, mfumo kuwepo kwa vifaa vya vizimamoto.
6. Wamiliki/waendeshaji ni lazima wawe wameandikishwa kwa mujibu wa sheria ya makampuni.
7. Mwombaji aeleze uzoefu wa kazi alizowahi kufanya.
8. Ombi la zabuni liwe na jina, anuani halisi la mwombaji na mahali Ofisi ilipo. (Physical address)
15. Maombi yaambatane na ada ya TShs. 100,000/= ambazo hazitarejeshwa kwa mwombaji. Fedha hizo zilipwe kupitia A/C Namba **01J1055955001 KAGERA COOPERATIVE UNION (1990) LTD** iliyopo CRDB
9. Tathmini itafanywa kwa kuzingatia vigezo 1-9 vilivyo tajwa hapo juu.
10. Barua za maombi zilizofungwa katika bahasha yenye lakiri na kuandikwa juu yake:-
"MAOMBI YA ZABUNI YA UTOAJI HUDUMA YA MAFUTA YA DIESEL NA PETROL KWA
MAGARI YA KCU MSIMU 2024/2025 kwa anuani tajwa hapa chini,
MENEJA MKUU,
KCU (1990) LTD,
P.O BOX 5,
BUKOBA.
11. Bahasha hiyo iletwe kwa mkono katika ofisi ya manunuzi KCU (1990) Ltd kabla au mnamo tarehe 19.04.2024. saa 4.00 asubuhi siku ya Ijumaa na ufunguzi wa maombi yote utafanyika muda huo, waombaji au wawakilishi wa waombaji wanaalikwa katika ufunguzi mara tu baada ya saa ya mwisho yakupokea zabuni
12. Maombi yatakayo chelewa, maombi yasiyokamilika, maombi yaliyowasilishwa kwa njia ya kieletroniki na maombi yasiyokuwepo siku ya ufunguzi hayatahusishwa na uchambuzi wa kumpata mzabuni.
Imetolewa na;

MENEJA MKUU
KCU (1990) LTD

